

LITANIA YA KUWAOMBEA MAPADRE WOTE 1

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 19, 2017

Sala za Katoliki: Sala Muhimu Kwa Mkristu Mkatoliki · #sala · #Sala - Litania · #Sala za Ibada

Kwa ajili ya Baba Mtakatifu wetu ..(N); Bwana, umpe moyo wako wa uchungaji mwema Kwa ajili ya warithi wa Mitume; Bwana, uwape wawe na uangalifu uliojaa upendo kwa mapadre wao Kwa ajili ya Maaskofu wako waliochaguliwa na Roho Mtakatifu; Bwana, uwabakishe karibu na kondoo wako Kwa ajili ya wachungaji wako; Bwana, uwafundishe kutumikia kuliko kutafuta kutumikiwa Kwa ajili ya waungamishi na washauri wa kiroho; Bwana, uwafanye kuwa vyombo visikivu kwa Roho wako Mtakatifu Kwa ajili ya mapadre wanaotangaza neno lako; Bwana, uwawezeshe kushirikisha Roho wako na Uzima wako Kwa ajili ya mapadre wanaosaidia utume wa walei; Bwana, uwatie moyo wa kuwa mifano bora Kwa ajili ya mapadre wanaofanya kazi na vijana; Bwana, uwajalie wawakabidhi vijana kwako Kwa ajili ya mapadre wanaofanya kazi kati ya watu fukara; Bwana, uwajalie wakuone na wakutumikie kupitia hao Kwa ajili ya mapadre wanaoangalia wagonjwa; Bwana, uwajalie wawafundishe thamani ya mateso Kwa ajili ya mapadre fukara; - Uwasaidie ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wagonjwa; - Uwaponye ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wazee; - Uwapatie tumaini la raha ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wenye huzuni na walioumizwa; -Uwafariji ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wanaohangaishwa na wale wanaosumbuliwa; - Uwape amani yako ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wanaodharauliwa na wanaonyanyaswa; - Uwatetee ee Bwana Kwa ajili ya mapadre waliokata tamaa; - Uwatie moyo ee Bwana Kwa ajili ya wale wanaosomea upadre; - Uwape udumifu ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wote; - Uwape uaminifu kwako na kwa Kanisa lako ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wote; - Uwajalie utii na upendo kwa Baba Mtakatifu na kwa maaskofu wao ee Bwana Kwa ajili ya mapadre wote; - Uwajalie waishi katika umoja na maaskofu wao ee Bwana Tunawaombea mapadre wote; - Wawe wamoja kama Wewe na Baba mlivyo wamoja ee Bwana Tunawaombea mapadre wote; - Waishi na kuendeleza haki yako ee Bwana Tunawaombea mapadre wote; - Washirikiane katika umoja wa ukuhani wako ee Bwana Tunawaombea mapadre wote, wakiwa wamejawa na uwepo wako; - Waishi maisha yao ya useja kwa furaha ee Bwana Tunawaombea mapadre wote; - Wajalie ukamilifu wa Roho wako na uwageuze wafanane nawe ee Bwana Kwa namna ya pekee, ninawaombea mapadre wale ambao kwa njia yao nimepokea neema zako. Ninamwombea padre aliyenibatiza na wale walioniondolea dhambi zangu, wakinipatanisha na Wewe na Kanisa lako. Ninawaombea mapadre ambao nimeshiriki Misa walizoadhimisha, na walionipa Mwili wako kama chakula. Ninawaombea mapadre walionishirikisha Neno lako, na wale walionisaidia na kuniongoza kwako. Amina.